



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI**



**TANGAZO LA KUKODISHA KARAKANA YA USEREMALA, GEREJI NA STOO KATIKA**  
**ENEO LA USADECO -SONI**  
**TAREHE 01/08/2023**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli anatangaza zabuni ya kukodisha karakana ya Useremala, Gereji na stoo kwa wafanyabiashara, Vikundi, Taasisi na watu binafsi ambao wangependa kukodisha maeneo hayo tajwa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kiujasiriamali.

Masharti ya jumla kwa watakaopenda kukodi katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

1. Wawe tayari kulipa kodi ya pango ya kukodisha eneo husika kila mwezi
2. Wasiwe wanadaiwa na Mamlaka za serikali ikiwemo Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli
3. Wataje kiwango cha malipo kama kodi ya pango kwa mwezi kwa eneo ambalo Watakuwa Wamechagua kukodi/Amechagua kukodi
4. Mwombaji/waombaji hawataruhusiwa kufanya shughuli nyingine tofauti na ile waliyoombea zabuni na si vinginevyo.
5. Barua za maombi ya kupangisha maeneo tajwa hapo juu ziambatane na ada ya maombi ya Tshs. 50,000/= [Hamsini elfu tu] na zilipwe kupitia akaunti namba 41610003118 miscellaneous Deposit NMB.
6. Mwisho wa kutuma maombi kwa waombaji/mwombaji ni tarehe **15/08/2023** siku ya Jumanne saa 4.00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa muda huo.
7. Mwombaji/waombaji watakaopenda wanaruhusiwa kushiriki kwenye shughuli za ufunguzi wa zabuni.

**HALI YA MAJENGO**

- A. **KARAKANA YA USEREMALA** – ina mashine moja mali ya Halmashauri kwa ajili ya kuchana mbao na inafanya kazi na stoo moja
- B. **STOO** – Zipo stoo 4 kwa ajili ya kuhifadhia vifaa mbalimbali kwa atakayehitaji kukodisha
- C. **ENEO LA GEREJI** – ina miundo mbinu rafiki kwa ajili ya utengenezaji wa magari mbalimbali yakiwemo mashimo pamoja na miundo mbinu ya umeme.

.....  
Baraka M. Zikatimu

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**BUMBULI**